



Unapojibu tafadhali taja:

Kumb. Na. NDC/L.20/5/76

02/09/2021

Meneja wa Kanda,

Kanda ya Nyanda za Juu Kusini,

Kituo cha Uwekezaji.

S.L.P 1316.

Mbeya.

YAH: KUMTAMBULISHA MWEKEZAJI WA KAMPUNI YA JIN SEN MU YE CO. LTD

Somo tajwa hapo juu la husika.

Ofisi ya Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Njombe inapenda kumtambulisha mwekezaji mtajwa hapo juu kama kichwa cha habari kinavyojieleza.

Mwekezaji huyu amekusudia kuweka kiwanda cha kuchakata mazao ya miti kwa ajili ya kutengeneza mbao za dari. (Ceiling Boards) Aidha eneo hilo la uwekezaji liko kwenye Kijiji cha Ikuna, Kata ya Ikuna na Wilaya ya Njombe. Eneo hilo lina ukubwa wa ekari 12 (Kumi na Mbili)

Taratibu za eneo hilo kutumiwa na mwekezaji huyo zimefanywa kwa mujibu wa sheria. kanuni na taratibu ikiwa ni pamoja na vikao ngazi ya Kijiji na Wilaya sambamba na ulipwaji wa fidia kwa wananchi ambao wakati wowote utatekelezwa kwani tayari mwekezaji amekwishaingiza fedha hiyo ya malipo ya fidia kwenye akaunti ya Halmashauri.

Kupitia barua hii ninaomba apewe ushirikiano na Taasisi yako ikimsaidia mwekezaji huyu kwa mahitaji ya kisheria ili kuona kwamba zoezi la uwekezaji linaanza mapema.

Asante kwa ushirikiano,

Chamulile Lucas Chigome

K.n.y: Mkurugenzi Mtendaji (W)

Halmashauri ya Wilaya ya Njombe.

**COY. MKURUGENZI MTENDAJI
WA WILAYA
NJOMBE**

Nakala:

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri (W): Aione kwenye jalada.